

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Baruapepe : [press@ikulu.go.tz](mailto:press@ikulu.go.tz)  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.

*Morogoro*  
*06 Agosti, 2024*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema kuwa Serikali imejipanga kurejesha ile hadhi ya kihistoria ya Mkoa wa Morogoro kuwa mkoa wa viwanda kwa kufufua viwanda na kuvutia uwekezaji mpya.

Rais Dkt. Samia ameyasema hayo wakati akihutubia wakazi wa Mkoa wa Morogoro katika Uwanja wa jamhuri akihitimisha ziara yake ya siku 5 kwenye Mkoa huo.

Aidha, Rais Dkt. Samia amesisitiza kuwa uwepo wa miundombinu ya reli na uwepo wa umeme wa uhakika kutoka Bwawa la Julius Nyerere unaufanya Mkoa wa Morogoro kuwa sehemu nzuri kwa uwekezaji.

Katika ziara yake Mkoani humo Rais Samia alitembelea uwekezaji wa upanuzi wa viwanda uliofanywa Mkoani humo ikiwemo Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa, na Kiwanda cha Sukari cha Kilombero.

Pamoja na mambo mengine, Rais Samia amesema kuwa upanuzi huo wa uwekezaji kwenye viwanda unampa imani kuwa ifikapo mwaka 2025/2026 Tanzania itakuwa katika nafasi nzuri ya kujihakikishia uzalishaji wa sukari kukidhi mahitaji yake.

Rais Samia pia amesema kuwa uwezekaji huo na upanuzi wa viwanda vilivyopo ni ishara kuwa Tanzania ina mazingira bora na yanayovutia kwa uwekezaji wa viwanda. Hivyo, ametoa rai kwa wakulima kuendelea kuzalisha kwa wingi ili kulisha viwanda vinavyojengwa.

Mapema leo, Rais Samia alizindua Kiwanda cha Sigara cha Serengeti (SCC) katika eneo la Kiwanda cha Uchakataji Tumbaku cha Mkwawa (MTPL) ambapo amepongeza uwekezaji huo ambao utakamilika Juni 2025, na kuzalisha ajira mpya 12,000 Mkoani Morogoro.

Sharifa B. Nyanga  
Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

